KUMB. Na.SSS/1105/F.I/2024/001

SHULE YA SEKONDARI KOMUGE,
S.L.P 250,
RORYA.
01/12/2023

JINA LA MWANAFUNZI ……………………………………..……
SHULE YA MSINGI ATOKAYO……………………………………
S.L.P 250,
RORYA.

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KOMUGE - RORYA**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2024 katika shule ya Sekondari Komuge. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 08/01/2024 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 22/01/2024. Ndani ya siku kumi na nne (14) usipofika,nafasi yako inaweza kuchukuliwa na mtu mwingine. Pia,kushindwa kufika/kuripoti kwako bila taarifa yoyote ya msingi kwa tarehe tajwa hapo juu, hatua za kisheria na za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako na mzazi/mlezi.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

## 2.1 SARE ZA SHULE.

- Mashati mawili (2) aina ya tetron/cotton meupe yenye mikono mifupi kila moja liwe na kola na Mfuko kushoto. Lazima yawe marefu ya kuweza kuchomekea na yasibane mwili. (kwa wote)
- Tai mbili, moja iwe ya damu ya mzee yenye mistari mieupe na nyingine iwe ya bluu yenye mistari mieupe kwa wanafunzi wote.
- Sweta (1) rangi nyeusi kwa ajili ya kujikinga na baridi kwa wote.
- Suruali mbili zenye tanapu na linda mbili kila upande, moja ya dark bluu na nyingine ya rangi ya damu ya mzee ( maroon ).Epuka kushona au kununua suruali zenye kubana ( modo ) haziruhusiwi kabisa (kwa wavulana).
- Mkanda mweusi usiwe na kichwa (chuma) kikubwa au mapambo mengine kwa wavulana.
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba jozi (2) visiwe vya boot na kisigino kirefu na soksi jozi (1) nyeupe na Nyeusi ( kwa wote)
- Fika na track suit rangi nyeusi yenye mistari mieupe, T- shirt rangi ya machungwa( orange) yenye nembo ya shule na kiatu cha raba (zitavaliwa wakati wa kipindi cha michezo).
- Sketi (2) aina ya tetron/cotton rangi ya dark blue na damu ya mzee (maroon), Marinda yawe ya kati(si madogo sana). Sketi zote ziwe ndefu zinazofika kwenye kifundo cha mguu (kwa wasichana).

**N.B. Sare zote zitakaguliwa siku atakaporipoti mwanao, hivyo anapaswa kufika nazo zote zikiwa zimekamilika na zisiwe na kasoro yoyote. Mzazi atalazimika kurudi nyumbani na mwanaye ikiwa sare za shule zitabainika kuwa na kasoro kama vile kuwa fupi, inayobana (modo) n.k hadi pale atakaporekebisha kasoro hizo.**

## 3.0 MAHITAJI MENGINE

a. Daftari kubwa 10 counter books Quire 2 na kuendelea kwa ajili ya notes za masomo yote.
b. Daftari ndogo 10 kwa ajili ya mazoezi ya darasani.

c. Afike na karatasi za kutosha ( **Ream moja aina ya DOUBLE- A**) kwa ajili ya kufanyia mitihani yake kwa mwaka mzima.
d. Mathematical set 1.
e. Dictionary moja ya kingereza kwa matumizi yake binafsi.
**f.** Afike na file 1 kwaajili ya kutunzia kumbukumbu zake za kitaaluma.
**g. Afike na kiti cha kukalia na meza ya kuandikia akiwa shuleni.**

**4.0 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA NI;-**

1. Wizi.
2. Uasherati, ubakaji na ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
4. Uvutaji Bangi.
5. Makosa ya Jinai.
6. Kupiga / Kupigana.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kuoa/ Kuolewa.
9. Kupata au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
10. Kutoa Mimba.
11. Kudharau Bendera ya Taifa.
12. Kugoma, Kuchochea na kuongoza fujo au kuvuruga amani na usalama shuleni.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Kukutwa na simu nje au ndani ya eneo la shule.

**5.0 WANAFUNZI WASITEMBELEE SEHEMU ZIFUATAZO ISIPOKUWA KWA KIBALI MAALUMU KUTOKA KWA MKUU WA SHULE/MWALIMU MHUSIKA**

a. Chumba cha mwalimu
b. Ofisi za shule;
c. Maabara
d. Jikoni
e. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu
f. Vilabu vya pombe
g. Majumba ya starehe mfano pool,vibanda vya sinema, saluni na sehemu za miziki
h. Majumba ya kufikia wageni (Guest House)

**6.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu, sayansi , teknolojia na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini.
Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ya muhimu na msingi;-

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c. Kushiriki kwa pamoja katika maandalio ya jioni (preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuiheshimu kwani kuwepo nje ya mipaka ya shule pasipokuwa na ruhusa ni kosa kubwa, hivyo heshimu mipaka ya shule kipindi chote cha uanafunzi wako.
f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule ni jambo la lazima.
g. Kuvaa sare ya shule inavyotakiwa muda wote inapokuwa mwilini mwako ni lazima.
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i. Kuheshimu kengere muda wote inapogongwa, itikia na kuwahi eneo husika.
j. Kutunza mali za umma ni lazima.

NB; **Mwanafunzi awapo Shuleni au Mtaani anapaswa kuheshimu sheria na taratibu za shule akiwa kama mwanafunzi. Kila mwanafunzi anapaswa kuripoti shuleni akiwa na kivuli cha cheti cha kuzaliwa.**

**SEHEMU YA MWANAFUNZI**

Mimi ………………………………………………………. ambaye nimechaguliwa kujiunga na masomo katika shule ya sekondari Komuge mwaka huu, Ninakili kuwa nimesoma na kuelewa vyema sheria na kanuni za shule na ninakubali kufuata sheria na kanuni hizo siku zote za uanafunzi wangu.
Saini ya Mwanafunzi ………………………………………Tarehe:…………………………..

**SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi……………………………………………………… naahidi kumlea mwanangu kulingana na sheria na kanuni za shule, na mwanangu amekubali kufuata sheria na kanuni zote za shule. Pia naahidi kushirikiana na walimu kumlea mwanangu ili kuleta mabadiliko chanya katika elimu yake.
Saini ya Mzazi/Mlezi………………………………..Tarehe:……….……………………………

**Hakikisha kuwa fomu ya afya imejazwa na kusainiwa na Mganga wa hospitali yoyote ya serikali inayotambulika na kuirejesha shuleni siku atakoporipoti mwanao.**

Karibu sana Komuge Sekondari

…………………………

**SAID NG'ONDA IDD**
**MKUU WA SHULE**
**0769 886 398**

**Kiambatanisho B**

## SHULE YA SEKONDARI KOMUGE

## MEDICAL EXAMINATION FORM

**( To be filled by an Authorized Government Medical Officer)**
**( Sharti ijazwe na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali)**

Full name ( Student) ……………………………………………………………………………

Age ……………………….. Height (in cms) …………………… Weight (in kgs) ……………………

1. Blood count ………………………………… ( Red and White) …………………………………..
2. Stool Examination ……………………………………………………………………………
3. Urine Analysis ………………………………………………………………………………
4. Syphilis and other V.D ………………………………………………………………………
5. T.B and Leprosy Test ………………………………………………………………………
6. Eye Test ……………………………………………………………………………………..
7. Ear Test ……………………………………………………………………………………….
8. ChestTest ……………………………………………………………………………………….
9. Abdominal Test ………………………………………………………………………………
10. Blood Group ( very crucial) ……………………………………………………………….
11. Spleen ……………………………………………………………………………………….
12. Additional Information eg. Physical Defect or Impairment, Infections, Chronic or Family Diseases(eg.Sicklecell) …………………………………………………………………………
    ……………………………………………………………………………………………………
    ……………………………………………………………………………………………………

I (full name ) ……………………………………………certify that the above student is fit/is not fit to pursue ordinary secondary education.

Designation …………………………. Station ……………………Signature ………………………..

Date ……………………………… Official stamp …………………………………………………....